## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI JULAI, 2023 NA MWELEKEO KWA MWEZI AGOSTI, 2023.

**Dondoo za tathmini ya Julai, 2023 na mwelekeo wa Agosti, 2023:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Julai, 2023 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Agosti, 2023 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 vipindi vya baridi vilijitokeza katika maeneo mengi nchini hususani nyakati za usiku na asubuhi. Vipindi vya baridi kali zaidi vilijitokeza katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na sehemu za miinuko za nyanda za juu kaskazini mashariki.
ii. Kwa mwezi Julai, 2023 vipindi vifupi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na maziwa makuu. Aidha, vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.
iii. Katika kipindi cha mwezi Agosti 2023, hali ya ukavu na baridi inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Ongezeko kidogo la viwango vya joto la chini linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini kuelekea mwishoni mwa mwezi. Vipindi vya upepo mkali pia vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 vipindi vya baridi viliendelea kujitokeza katika maeneo mengi nchini hususan nyakati za usiku na asubuhi. Vipindi vya baridi zaidi vilijitokeza katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Viwango vya chini zaidi vya joto kati ya nyuzi joto 2 °C na 9 °C viliripotiwa katika maeneo ya Igeri (Njombe) na Uyole (Mbeya). Aidha,

vipindi vifupi vya upepo mkali unaofikia kasi ya km 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, husussan ukanda wa pwani na maziwa makuu. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani na sehemu za miinuko za nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI AGOSTI, 2023

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2023 joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la juu ya wastani. Aidha, eneo la magharibi mwa bahari Hindi linatarajiwa kuendelea kuwa na joto la bahari la juu ya wastani na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi, joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Kwa upande mwingine, hali ya joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, joto la bahari la juu ya wastani katika ncha ya kusini mwa Afrika linatarajiwa kuendelea. Hali hii inatarajiwa kupunguza uwepo wa hewa yenye ubaridi kutoka kusini na hivyo kusababisha vipindi vichache vya baridi zaidi nyakati za usiku katika baadhi ya maeneo, hususani ukanda wa Pwani.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2023

Mwelekeo wa hali ya hewa kwa kipindi cha mwezi Agosti 2023, unaonesha kuwa maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuendelea kuwa makavu pamoja na hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na maeneo machache ya ukanda wa Ziwa

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

Victoria na sehemu za miinuko za nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali unaofikia kasi ya km 40 hadi 50 kwa saa vinatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, kati, nyanda za juu kusini magharibi na maziwa makuu. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 21 °C hadi 26 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Kwa maeneo ya nchi kavu, viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C na 20 °C. Kiujumla hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, hususan wiki ya kwanza na ya pili.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 19 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Maeneo mengi yanatarajiwa kuwa na viwango vya joto la chini kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C. Aidha, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko, ikijumuisha mkoa wa Njombe, yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi zaidi kwa viwango vya chini ya nyuzi joto 8 °C. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 17 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Kiujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya mwambao wa pwani, hususan wiki ya kwanza na ya pili.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 12 °C. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

### 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2023 mifumo ya hali ya hewa inaonyesha kuendelea kwa hali ya ukavu katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache. Kwa upande mwingine, ongezeko kidogo la joto linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini.

### 2.4 USHAURI

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Agosti, 2023 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz